HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi :255(28) 2501375
Ofisi zote :255 (28) 40334
Fax :255 (28) 2500785
E-mail.mwacity@thenet.co.tz
"Unapofibu Tafadhali Nukuu:

S. L.P. 1333
MWANZA.
TANZANIA

WASIMAMIZI WASAIDIZI WA UCHAGUZI,
MAJIMBO YA NYAMAGANA NA ILEMELA,
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA.

18/10/2010

YAH : UTEKELEZAJI WA HARAKA KUHUSU MAAGIZO YAFUATAYO :-

Tafadhali husikeni na kichwa cha habari hapo juu,

Kutokana na hali halisi ya kisiasa iliyopo hivi sasa katika majimbo yote mawili katika Halmashauri ya jiji la Mwanza na Taifa kwa ujumla hali si nzuri hata kidogo. Ili kunusuru ngazi za Kata, majimbo na Taifa kwa ujumla kwenda na upinzani, katika kikao cha ndani tulichokaa tarehe 16/10/2010, LA - KAIRO HOTEL na waheshimiwa waandamizi na makada wa chama cha mapinduzi jumla ya watu 30, kwa kutaja baadhi.

- Mhe. J.K Kikwete
- Mhe. Rostam Azizi
- Mhe. Edward Lowasa
- Ndugu.Christopher M. Gachuma
- Ndugu.Ridhiwani Kikwete

Tuliazimia kwa pamoja maazimio yafuatayo:-

Ili yaweze kutekelezwa mara moja ikiwa ni mikakati mbadala na thabiti ili kujihakikishia mazingira mazuri ya ushindi wa Chama katika uchaguzi huu Mkuu.

1. Kupunguza na kutobandika idadi kubwa ya Vijana waliojiandikisha kupiga kura katika vituo husika vya kupigia kura kwani inaaminika ndio walio wengi katika kambi ya upinzani ili wakose fursa ya kupiga kura.
2. Kucheleweshe kubandika majina ya wapiga kura katika vituo vya kupigia kura (zoezi la kubandika lianze tarehe 24/10/2010 badala ya tarehe 20/10/2010 kama ilivyo pangwa awali)

3. Kuhakikisha kuwa kuna kuwepo na vituo hewa angalau (3-4) katika kila kata na kutopiga mihuri nyuma kwa baadhi ya karatasi za kupigia kura kwa kadri mazingira yanavyoruhusu.
4. Kutoa taarifa mara moja kwa vyombo vya dola (Polisi) kutovumilia vikundi vya watu hasa mara baada ya kupiga kura na kuwatawanya.
5. Kucheleweshe utangazaji wa matokeo na uwepo wa dola wakati wa kutangaza matokeo.
6. Kupata wasimamizi wa vituo, na wasaidizi, na makarani ambao ni Wanachama na makada wa chama cha mapinduzi ili waweze kukinusuru chama kwa hali yoyote iwayo.
7. Kuhakikisha Green Guard inatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa maelekezo yatolewayo.

NB: Ripoti na taarifa zilizotolewa na wenyeviti, makatibu na makamanda wa Wilaya waliotembelea na kusikiliza mawaidha na kampeni za ndani ya misikiti na Kanisani zinafanyiwa kazi kwa utekelezaji.

Aidha zoezi hili linapaswa kutekelezwa kwa usiri na umakini wa hali ya juu, sambamba na utoaji wa taarifa .

Nakutakieni utekelezaji mwema.

M. W. KABWE
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA